# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# MKOA WA KAGERA
# HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA
# SHULE YA SEKONDARI KYERWA

## MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KYERWA JULY, 2024

**MKUU WA SHULE 0622279831**

**MAKAMU MKUU WA SHULE 0629288212/0764489120**

**MATRON/PATRON 0684938598**

**SHULE YA SEKONDARI KYERWA,**

**S. L P 160,**

**KYERWA.**

**28/06/2024**

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

**...................................................................**

**S. L. P ..........................................**

**.......................................................**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KYERWA HALMASHAURI YA WILAYA KYERWA MKOA KAGERA MWAKA 2024.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya PCM. Shule ya sekondari KYERWA umbali wa kilometa 0.5 kutoka Halmashauri ya wilaya Kyerwa. Usafiri wa bodaboda ni tsh 1000/= tu hadi shuleni.

   Muhula wa masomo unaanza tarehe 1/7/2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 28/06/2024 mwisho wa kuripoti ni tarehe 6/07/2024.
2. Mambo muhimu ya kuzingatia:

   2.1 Sare za shule

   i. Sare ya shule hii ni sketi mbili (2) Rinda box (Rinda moja kubwa mbele na nyuma na mawili kwa kila upande (sketi ziwe na rangi ya light blue). Sketi zinatakiwa ziwe ndefu kiasi cha kufunika magoti.
   ii. Mashati mawili (2) mikono mirefu (Rangi nyeupe)
   iii. Hijabu mbili rangi nyeupe zifunike kifua cha mwanafunzi pia ziwe ndefu kufikia kifundo cha mikono akisimama (kwa waislamu)
   iv. Sare ya michezo ni track suit moja rangi ya blue yenye michirizi nyeupe na viatu vya raba vinavyofungwa na Kamba.
   v. Viatu vya shule ni nyeusi vya kufunga na Kamba vyenye visigino vifupi.
   vi. Soksi jozi mbili nyeupe za shule (stocking)
   vii. Sweta moja rangi light blue yenye michirizi nyeupe shingoni na mikononi pamoja na kiunoni
   viii. Nguo za kushinda (shamba dress) ni magauni mawili marefu kitambaa cha kunguru draft rangi nyekundu.
   ix. Tai rangi ya blue yenye mistari nyeupe.
   x. Tisheti ya kijivu pote yenye kola.

(MAVAZI YOTE PICHA ZIMEAMBATANISHWA MWISHONI)

N.B: MWANAFUNZI HARUSIWI KUVAA NGUO TOFAUTI NA ZA SHULE MDA WOTE AWAPO SHULENI

2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:

i. Madaftari nane (8) (COUNTERBOOKS QUIRE 3)
ii. Ream (A4) 2 ya karatasi kwa mwaka mmoja kila muhula
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatishwa)

iv. Scientific calculator (ORIGINAL)
v. Godoro liwe na vipimo futi 21/2 upana na futi 6 urefu
vi. Mashuka jozi 2 (rangi pink), blanket 1 (rangi yoyote), chandarua 1 na mto mmoja
vii. Nguo za ndani za kutosha
viii. Vyombo vya chakula 9sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
ix. Ndoo 01 ndogo (lita 10) ndoo kubwa 01 lita 20 iliyoisha rangi au iliyoisha mafuta lita 20 zenye mifuniko.
x. Beseni 1 kwa ajili ya kuoga na kufulia.
xi. Dumu moja la lita 5 jeupe kwa ajili ya kutunza maji ya kunywa
xii. Kwanja I, jembe 1, mundu 1, mifagio 2 wa ndani na wa nje
xiii. Kila mwanafunzi anapaswa kuja na bima ya afya kwa ajili ya matibabu iwapo ataugua.
xiv. Spring File 2
xv. Graph pad 01
xvi. Picha 2 aina ya passport size zenye background ya kitambaa cha blue
xvii. Cheti cha kuzaliwa (BIRTH CERTIFICATE)
xviii. Hati ya matokeo (Results slip)

2.2 MICHANGO MBALIMBALI

| NA | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000 |
| 2 | Tahadhari | 5,000 |
| 3 | Nembo | 5,000 |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000 |
| | **JUMLA** | **80,000** |

Malipo ya michango hii yalipwe kupitia account ya shule ambayo 31906600239
Jina: **KYERWA SECONDARY SCHOOL RE- CURRENT (NMB)**

## 3. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu na 25 ya mwaka 1977.aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini.unatakiwa kuzingatia kanuni na sheria hizi kwa kipindi chote utakachokuwa hapa .(maelekezo mengine utapewa mara ufikapo shuleni)

1. Kila mwanafunzi ni lazima kuvaa nguo rasmi za shule (school uniform) wakati wote awapo shuleni,na mahali pengine atakapotakiwa kufanya hivyo
2. Ni muhimu na wajibu kwa kila mwanafunzi kuwahi bila kuchelewa mahali popote utakapohitajika darasani,kazini,mstarini nk
3. Juhudi katika kazi za mikono,madarasani na katika michezo ni wajibu wa kila mwanafunzi.uzembe katika shughuli hizi hauruhusiwi kabisa

4. Kila mwanafunzi wa shule hii ni lazima aombe ruhusa endapo atakosa kuwepo shuleni.hata hivyo mwanafunzi atalazimika kurudi shule kabla ya saa 11:50 jioni kila inapotokea kuwa nje ya shule kwa sababu yoyote ile
5. Kila mwanafunzi ni wajibu kujiheshimu yeye binafsi na kuwaheshimu watu wengine kama wanavyopenda kuheshimiwa
6. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kutunza na kulinda siha na usafi wake binafsi (usifuge ndevu,nywele ndefu,kucha n.k)
7. Vitendo vyovyote vya kushiriki au kushawishi mgomo wa aina yoyotr shuleni ni marufuku kabisa
8. Ugomvi au kupigna, kuleta fujo madarasani.lugha za matusi,kashfa kwa wenzake au wananchi ni mwiko kabisa
9. Vipindi vyote vilivyoko kwenye ratiba ni lazima uvihudhurie bila kukosa pamoja na shughuli za nje ya darasa
10. Kila mwanafunzi sharti aepuke na kuchukia vitendo vyovyote vya uongo,uzushi,wizi,uasherati,ulevi,uvutaji sigara na uchoyo
11. Upole na utii kwa viongozi ni wajibu kwa kia mwanafunzi:ubishi wenye lengo la kukwepa kutiiza wajibu ni marufuku kabisa
12. Makoti,vibandiko,vizibao,kofia,kandambili,viatu vya wazi,mikanda mipana haviruhusiwi kamwe kuvaliwa wakati mwanafunzi awapo ndani ya vazi la shule
13. Lugha inayotumika hapa shuleni ni kiingeleza tu
14. Kutimiza kwa makini maandalizi ya jioni (preparation)
15. Ni marufuku kuwa na simu ya mkononi (mobile phone) chip(line) earphone / headphone charger powerbank kompyuta (laptop) i pad,pasi ya umeme,heater za umeme,redio,kondomu,n.k usije navyo shuleni.
16. Ni marufuku kupeleka chakula mabwenini
17. Ni marufuku kumiliki kifaa chochote kinachoweza kusaidia kufanya biadhara shuleni au kufanya biashara yoyot mwanafunzi awapo shuleni. Mfano kamera kuuza vyakula au vinywaji n.k
18. makosa yafuatayo yaweza kukufanya ufukuzwe ama kutolewa shuleni
    a) Wizi
    b) Ulevi au unywaji wa pombe,uvutaji wa sigara na matumizi ya madawa ya kulevya kama uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kubeli n.k

c) Ubakaji
d) Kudharau bendera ya taifa
e) Kuoa au kuolewa
f) Kuharibifu wa makusudi wa mali ya umma
g) Kuoma kuchochea na kuonoza au kuvuruga amani na usalama wa shule
h) Kukataa adhabu kwa makusudi
i) Kupigana na kupiga
j) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa /utoro wa masomo
k) Kushawishi / kushiriki katika migmo
l) Kutofanya mitihani na mazoezi
m) Mapenzi ya ngono na wanafunzi wenzake shuleni au watu wengine nje ya shule (uasherati na ushoga
n) Kumpa mimba mwanafunzi wa kike mimba
o) Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi au kifaa chochote kinachohusiana na simu
p) Kushiriki matendo ya uhalifu siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
q) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
r) kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiuwa kwa kunywa sumu n.k
s) Kupanga /kuishi mtaani ukkiwa shuleni /wakati wa masomo
t) Kutenda tendo lolote lisilokuwa la kawaida shuleni au nje ya shule

**3.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (preparation)
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani nan je ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
ix. Kutunza mali za shule.
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari, na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa mkuu wa shule. (msiba au ugonjwa).**

3.2 Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na:

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa Zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa mwanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yoyote yule.
**vi.** **Kusuka nywele kwa mitindo usiokubalika**. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au **kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.**
vii. Uvutji wa sigara
viii. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa.
ix. Kupata ujauzito au kutoa mimba.

x. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sharia za nchi.
xi. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
xii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xiii. Kudharau Bendera ya Taifa.
xiv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu, na
xv. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

3.Viambatanisho na fomu muhimu

i. Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.
ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu Historia ya mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makossa ya jinai.na
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sharia, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule, na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa wanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

4. Tafadhari soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBUNI SANA SHULE YA SEKONDARI KYERWA**

Saini ya Mkuu wa shule ............................................

Jina la Mkuu wa shule OMBENI AYRO GURTI

Mhuri wa Mkuu wa shule ........................................

N.B Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa nia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO**

- MKUU WA SHULE: 0622279831/0786476231
- MAKAMU MKUU WA SHULE:0629288212/0764489120
- MWANDAMIZI TAALUMA:0762052274
- MWANDAMIZI MALEZI: 0762052274

## SHULE YA SEKONDARI KYERWA
## FOMU YA KUKUBALI NA KUTII SHERIA ZA SHULE

ANWANI …………………………………………...
Mimi ……………………………………………………. (Jina la mwanafunzi) nimepokea barua ya kuingia kidato cha Tano katika shule ya sekondari KYERWA kuanzia tarehe 01/07/2024 hadi 06/07/2024. Nakubali nafasi hiyo kwa moyo mkunjufu. Baada ya kusoma na kuelewa sheria za shule, naahidi kuwa nitatii sheria hizo kama zilivyoainishwa katika fomu ya maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari KYERWA. Endapo nitashindwa kutii sheria hizo hatua inayostahili ichukuliwe dhidi yangu
Natoa ahadi hii mbele ya Mzazi /mlezi wangu ambaye ametia sahihi yake hapa chini.
Jina la mwanafunzi ……………………………………….. sahihi…………………
Mimi………………………………………….. (Jina la mzazi /mlezi) ambaye ni mzazi /mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu, nakubali mwanangu ajiunge kidato cha Tano katika shule ya sekondari KYERWA na kutii sheria za shule na naahidi kushirikiana na shule ili kuhakikisha tunatoa malezi bora kulingana na sheria hizo na nyingine ambazo hazikutajwa pia.
Iwapo sitakuwepo mimi likitokea tatizo ninaweza kuwakilishwa na
1. …………………………………………... ambaye ni ……………………………….
2. …………………………………….. ambaye ni …………………………………….
(Eleza uhusiano wako na wawakilishi hao)………………………………………..
Sahihi ………………………………
Tarehe………………………………………………………………

## SHULE YA SEKONDARI KYERWA
## KIAMBATANISHO B
## MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. JINA KAMILI …………………………...................................... (Kama ilivyo kwenye kadi ya maendeleo shuleni)
2. Tarehe ya kuzaliwa ...............................
3. Mahali alipozaliwa: Wilaya……………… Kijiji ………………….. kata …………
4. Anwani ya nyumbani ni ……………………………………………………..
5. Dini yake ……………………………………………..

**WAZAZI**/MLEZI
Jina ……………………………………......... Anwani …………………………………..
Anaishi /Amefariki (kata isiyohusika)……………………………………….
Ni Raia wa nchi ipi? Itaje ................................................ (Tanzania/nchi nyingine)

**MAELEZO YA AFYA**

Eleza kama una tatizo lolote linalohitaji msaada au linaloweza kuathiri utendaji wako wa kazi za kila siku pamoja na maendeleo yako ya masomo. Maombi maalumu yadhibitishwe na daktari.
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA**
**SHULE YA SEKONDARI KYERWA**
**S.L.P 160 KYERWA**

## FOMU B:HATI YA UTHIBITISHO WA MGANGA

Tafadhali mpime Mwanafunzi……………………………………………………

na utujulishe afya yake kuhusiana na :-

a) Kinyesi…………………………………Matokeo ………………………………
b) Mkojo…………………………………Matokeo………………………………
c) Macho…………………………………Matokeo………………………………
d) Damu ………………………………… Matokeo………………………………
e) Mapigo ya Moyo………………………Matokeo………………………………
f) Kifua Kikuu……………………………Matokeo………………………………
g) Vidonda vya Tumbo……………………Matokeo………………………………
h) Pumu…………………………………Matokeo………………………………
i) Mimba …………………………………Matokeo………………………………
j) Na matatizo mengine……………………………………………………………

Nathibitisha kuwa Mwanafunzi……………………………………………………

Afya yake ni hafifu / anastahili matibabu yafuatayo…………………………

afya yake ni nzuri anaweza kuendelea na masomo ya sekondari………………

……………………………………………………………………………………………

Jina laMganga …………………………Sahihi……………………………

Muhuri………………………………Tarehe……………………………

*ombeni gurti*

……………………………………
**OMBENI AYRO GURTI**
**MKUU WA SHULE**

**SHULE YA SEKONDARI KYERWA**

**KIAMBATANISHO CHA MAVAZI YA SHULE**

| | | |
|---|---|---|
|  |  |  |
| **Sweta na Sketi** | **Shati na Tai** | **Hijabu** |
|  |  |  |
| **Sare za Michezo** | **T-shit** | **Shamba dress** |